## KUKATA MAUA KWA WAKATI UNAOFAA (TOPPING)

Mkulima anashauriwa kukata maua baada ya asilimia 50 ya mimea yote kuchanua na kufungua maua. Kitendo cha kukata maua ni kutaka majani yahifadhi wanga unaotengenezwa na kufanya tumbaku kuwa nzito. Vinginevyo wanga huo utatumika kutengeneza mbegu za tumbaku na kufanya majani ya tumbaku kuwa mepesi. Aidha, ukataji wa maua unasaidia kurefuka kwa majani na mizizi kuongezeka. Idadi ya majani yanayohitajika katika mmea ni 16-18 kulingana na lishe ya mmea.

## KUONDOA VIKONYO

Mara baada ya kukata maua, mmea huanza kutoa vikonyo (matoto). Vikonyo hutumia akiba ya wanga ili kukua. Hivyo havina budi kuondolewa kabla havijafikia urefu wa nchi 2. Vikonyo huondolewa kwa mikono au kwa kutumia dawa ya kuzuia vikonyo wakati wa kukatia maua.

## MAGONJWA NA WADUDU

Magonjwa ambayo huathiri sana tumbaku ni dumping off, rossete, anthracnose na brown spot na wadudu wanaoshambulia sana tumbaku ni nzi weupe, nematode, minyoo ya kukata na mchwa, wadudu hawa hasa hushambulia miche ikiwa bado kwenye kitalu.

## UVUNAJI

Kabla mkulima hajaanza kuvuna tumbaku ni lazima ahakikishe mabani ya kukaushia yako katika hali nzuri ya kuanza kazi ya ukaushaji.

Mkulima anatakiwa avune majani yaliyokomaa tu na siyo majani machanga. Dalili za jani lililokomaa ni kubadilika kwa jani, kutoka kijani kibichi kwenda kwenye kijani chepesi. Ncha za jani itaanza kuonekana kama njano na jani litainama kidogo.

Ni kawaida ya jani la tumbaku kuwa na mafuta ambayo hunata, hivyo jani lililokomaa litakuwa na mnato kidogo sana na vinyweleo havitakuwepo.

Mkulima anashauriwa atofautishe kati ya jani la kawaida na jani la mmea uliokosa lishe kwa vile majani yaliyokosa lishe yataonekana kama yamekomaa kumbe sivyo.

Mkulima anashauriwa avune tumbaku yake kati ya asubuhi na saa tano kwa vile jua la mchana hufanya majani ya tumbaku yaonekane kama yamekomaa kumbe sivyo. Katika masaa hayo pia majani ya tumbaku hayawezi kunyauka kwa urahisi jambo ambalo lingeleta tatizo kwenye ukaushaji. Tumbaku isivunwe ikiwa imenyeshewa mvua. Vuna siku ambayo mvua haijanyesha.

## UCHAMBUZI WA TUMBAKU

Wakulima wengi wanajiuliza ni kwanini kuwepo na madaraja mengi ya tumbaku. Wengine wanafikiri kuchambua tumbaku kulingana na madaraja ni kumsumbua mkulima na kumpotezea wakati.

Ukweli ni kwamba uchambuzi wa tumbaku unafanywa ili kukidhi mahitaji ya mtumiaji (Mvutaji sigara). Kuna wavutaji wa sigara baridi na wavutaji wa sigara kali. Kwahiyo, uchambuzi wa majani ya tumbaku kulingana na madaraja unamrahisishia mtengenezaji wa sigara aweze kufanya uchanganyaji (Blending) kufuatana na mahitaji ya mteja wake. Hivyo basi, mkulima kabla hajapeleka tumbaku yake sokoni sharti aichambue na kuifunga kwenye vishada na mitumba kwa kuzingatia michumo, ubora, rangi, dosari na hata urefu wa majani.

Kwa maana nyingine, mkulima afunge tumbaku kwenye vishada na kwenye mitumba kulingana na zinavyofanana misingi ya hapo juu.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA KILIMO**

# BODI YA TUMBAKU TANZANIA

# KILIMO BORA CHA TUMBAKU

## WASILIANA NASI:


Mkurugenzi Mkuu,
Bodi ya Tumbaku Tanzania,
5 Barabara ya Kihonda Maghorofani - Bima,
S.L.P 227,
**67128 MOROGORO - TANZANIA.**
**Barua Pepe:** info@tobaccoboard.go.tz
**Tovuti:** www.tobaccoboard.go.tz

## UTANGULIZI

Tumbaku huzalishwa kwa ajili ya majani yake,majani ya tumbaku yanapo komaa huvunwa na tumbaku hutumika hasa kutengeneza sigara. Aina za tumbaku zinazo limwa Tanzania ni Tumbaku ya Mvuke *(VFC)*, Tumbaku ya Moshi (*DFC*) na Tumbaku ya Hewa (Burley). Tumbaku ya Moshi hulimwa kusini mwa Tanzania hasa Ruvuma na Tumbaku ya Mvuke hulimwa Tabora, Shinyanga, Kigoma, Katavi, Iringa, Mbeya, Songwe, Singida, Morogoro, Mara, Kagera na Geita. Tumbaku ya Hewa (Burley) hulimwa katika mikoa ya Ruvuma, Geita na Kagera.

Aidha, kwa sasa tumbaku mpaya aina ya Dark Air Cured inafanyiwa majaribio katika mkoa wa Iringa.

## HALI YA HEWA NA UDONGO

Tumbaku inahitaji kiasi cha 38mm cha mvua ambayo imenyesha vizuri katika kipindi cha wiki 16 baada ya kupanda au kuhamishia miche shambani (transplanting). Mvua nyingi huwa na madhara na huchochea kupatikana kwa magonjwa.

Tumbaku ya mvuke husitawi vizuri katika udongo mwepesi (*loamy*) na udongo wa kichanga (*sandy*), na haihitaji udongo unao tuamisha maji na pia inahitaji Nitrojeni katika hatua za mwanzo na kadri inavyo zidi kukua uhitaji wa nitrojeni hupungua. Udongo unapokuwa na nitrojeni nyingi wakati wa majani kukomaa ubora wa majani hupungua.

Tumbaku husitawi vema katika maeneo yenye mwinuko toka usawa wa bahari m 900 hadi m 1500, japokuwa Tumbaku ya moshi haistawi vizuri kwenye maeneo yenye mwinuko m 1400 kutoka usawa wa bahari.

## MBEGU ZA TUMBAKU

Mbegu za tumbaku ya mvuke zinazolimwa nchini Tanzania ni K326, RG17, ULTF10 na DDV10 na kwa tumbaku ya moshi aina inayolimwa Tanzania ni *heavy western*.

## KUTENGENEZA VITALU

Zingatia kutafuta eneo zuri na salama la kuweka vitalu na lazima liwe karibu na chanzo cha maji, kama eneo lipo sehemu ambayo kuna upepo mkali zingatia kutengeneza kikata upepo. Badilisha upande wa kuweka vitalu kila mwaka kuzuia wadudu waharibifu (*Nematodes*).

Tengeneza vitalu vilivyo inuka viwe na upana wa m 1.2 na urefu wa m 23. Baada ya kutengeneza matuta tifua udongo uwe katika size ndogo na baada ya hapo nyunyizia dawa ya kuuwa nematode kwa kufuata maelezo kwa usahihi yaliyo andikwa katika chupa ya dawa.

Kabla ya kupanda weka mbolea ya NPK10:18:24 katika vitalu ukichanganya na udongo kwa kutumia reki, na baada ya kuweka mbolea chukua keni na weka maji safi ndani yake kisha weka mbegu ndani ya keni hiyo na kisha nyunyizia maji na mbegu katika kitalu kwa usahihi na baada ya hapo changanya kwa kutumia reki tena.

Baada ya maelekezo hapo juu, wekea nyasi vitalu vyako na kisha mwagilia kila siku mara tatu na utatoa nyasi hizo pale unapoona mbegu zimeanza kuota kuanzia wiki ya 3 na kuendelea.

Baanda ya mbegu kutokeza na kuondoa nyasi unamwagilizia mara moja kwa siku na wiki 2 kabla ya kuhamishia miche shambani mwagilia mara 1 kwa siku mbili ili kuwezesha miche kuhimili ukame, na miche hua tayari kwa kuhamishiwa shambani baada ya wiki 8 toka kupandwa.

Hamishia miche shambani inapofikisha urefu wa sm 15 na zingatia usafi wa mikono na mavazi wakati unafanya kazi katika vitalu vya tumbaku na pia epuka kuvuta sigara ukiwa shambani.

## KUANDAA SHAMBA

Tengeneza matuta yenye umbali wa m 1, pia zingatia kuzika magugu yote na tengeneza matuta mapema katika kipindi cha mvua ukifanya hivyo itasaidia kuhamishia miche shambani mapema katika kipindi cha mvua.

## KUPANDA

Tumbaku hupandwa kwa kutumia mbegu, mbegu hupandwa katika vitalu na huhamishiwa shambani pale inapo fikisha urefu wa sm 15.

Mwagilia miche wakati wa asubuhi au jioni na ng'oa miche kwa umakini ili kuepusha kukata mzizi mkuu (*tap root*).

Tengeneza mashimo katika matuta na kama unapanda tumbaku ya moshi mashimo yanatakiwa kuwa na umbali wa 1m na kama unapanda tumbaku ya mvuke umbali wa mimea huwa sm 50 hadi sm 60 na kama mashimo ni makavu mwaga lita 1 hadi 2 za maji kwa kila shimo, zingatia kuacha mzizi mkuu ukiwa wima.

## PALIZI

Usafi wakati wote unasisitizwa sana kuepusha ushindani kati ya tumbaku na magugu kupata maji na viini vya mbolea. Ni jambo la lazima kutifulia tumbaku kulegeza udongo karibu na mimea ya tumbaku na kujenga tuta upya kuwezesha mmea kunyonya lishe ya kutosha katika kipindi kuanzia wiki ya 4 hadi 6 baada ya kupanda ambapo tumbaku hukuza shina haraka haraka

## MBOLEA

Weka mbolea ya NPK10:18:24 wiki moja baada ya kupanda na unatakiwa kuweka kina cha 10cm na umbali wa 10cm toka kwenye mmea. Baada ya wiki ya tatu tangu kupanda weka mbolea ya kukuzia CAN 26-27% Nitrojeni ili kupata majani mazito.